HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI KIUSA

S.L.P. 8229 MOSHI.

Mob: 0754916960 **Barua pepe:** kiusasecondaryschool@gmail.com

Tarehe.....

Jina la mwanafunzi.....
.....
S.L.P.....
.....

YAH: FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIUSA WILAYA YA MOSHI(M) MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021

1.0 Utangulizi:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika Shule ya Sekondari Kiusa **mwaka 2021, HONGERA SANA!**. **Shule ya Sekondari Kiusa** ipo umbali wa **km 0.5** Magharibi mwa **Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.**

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza **tarehe 11/01/2021.** Unatakiwa kuripoti shuleni **tarehe 11/01/2021 saa 1:00 Asubuhi** na mwisho wa kuripoti shuleni ni **tarehe 15 /01/2021**.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

Wavulana sare ya shule hii ni **SURUALI mbili (2)** za rangi ya **Karoti** zenye marinda mawili, mbele mfuko moja nyuma, turn up na upana wa mguu usiopungua inchi 16.

Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino cha kawaida na kamba, Sweta rangi **Nyeusi** na Soksi jozi mbili nyeupe **(sio stocking)**

Wasichana **SKETI mbili (2)** za rangi ya **Karoti** zenye mshono wa **Rinda Box. (Sampuli ya kitambaa imeambatishwa)**

Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino cha kawaida na kamba, Sweta rangi ya **Nyeusi** na Soksi jozi mbili nyeupe **(sio stocking)**

Picha za passport size za mwanafunzi **(2)** na za mzazi **(2).** Wavulana wavae vesti nyeupe na Wasichana wavae vesti nyeupe au nyeusi.Wavulana wavae mikanda rangi nyeusi ya ngozi isiyo na **bakoli** kubwa.

NB: Mashati meupe mawili **(2)** mapya ya mikono mifupi kwa wasichana na wavulana.

a) Wasichana wa **dini ya Kiislam** ni lazima kuvaa **stara** kama mchoro uliyoambatishwa unavyoonesha.

Shorti kanzu ya cotton nyeupe au halua nyeupe ya kuvaliwa kwa skirt ndefu na sio suruali yenye kufunika mfuko wa skirt. (Rangi ya skirt ifanane na sampuli iliyoambatishwa).

Kitambaa cha **shungi** kiwe cha cotton nyeupe au halua nyeupe na **sio blue.**

b) **Sare ya michezo kwa shule hii ni: Kwa Wavulana -** Bukta ya rangi nyeusi na T-shirt rangi ya Blue na **kwa Wasichana-** track ya rangi nyeusi na T-shirt ya rangi ya blue.

2.2 MAHITAJI YA MASOMO

a) Daftari 9 ambazo ni Counter book Quire 2 pamoja na daftari ndogo 9 za mazoezi.
b) Kalamu za wino na za risasi pamoja na mkebe wa Hisabati.
c) Kamusi ya Kiingereza kwa kiingereza.
d) Saa ya mkononi ni lazima kwa kila mwanafunzi (inajenga nidhamu binafsi ya kutunza muda).
e) Begi la shule lisilo na madoido au picha (mifuko ya plastiki/rambo hairuhusiwi)

NB. Mzazi ajenge utamaduni wa kumnunulia mwanae vitabu vya ziada na kiada kwa ajili ya rejea zaidi kwani shule haina uwezo wa kuwapa wanafunzi wote vitabu.

2.3. CHAKULA/NAULI/MATIBABU

Chakula cha mwanafunzi, nauli ya kwenda na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni jukumu la mzazi/mlezi wa mwanafunzi, hivyo kila mzazi/mlezi anapaswa kutimiza wajibu wake.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za Shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na. 25** ya **mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **Sheria Na. 10** ya mwaka **1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na **Ofisi ya Rais – TAMISEMI** yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatatolewa ufafanuzi kwenye vikao vya wazazi/wanafunzi.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
h) Kutunza mali za umma.
i) Ni marufuku mwanafunzi kuvaa kandambili au viatu vya wazi anapokuwa shuleni.
j) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia lugha ya matusi au za mtaani awapo shuleni/ nje ya shule.
k) Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda au kuonekana kwenye sehemu za starehe kama Bar, Disco na nyumba za wageni (Guest house) nyumba za starehe.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito / kupata mimba/kusababisha mimba.
i) Kuoa au kuolewa, au kuwa na mahusiano ya kimapenzi nje na ndani ya shule.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza maandamano au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

m) Kuwa na simu ya mkononi.
n) Utoro wa jumla au rejareja.
o) Kuwa na tatuu (Tattoo) au kupatikana na mchoro wa tatuu (tattoo).

3.2 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Fomu ya mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

3.3 USAFI BINAFSI

Ni lazima mwanafunzi awe nadhifu kila wakati, anyoe nywele zake kwa staha(ziwe fupi muda wote) **SI RUHUSA KWA MWANAFUNZI WA KIKE KUSUKA.**
Si ruhusa kufuga ndevu, kufuga kucha na kupaka rangi kucha au hina.

4.0 UTARATIBU WA MASOMO

Siku za masomo ni kila siku ya Jumatatu mpaka Ijumaa. Mwanafunzi analazimika kufika shuleni saa moja kamili **asubuhi(1:00)** kwa ajili ya "roll call", usafi na matangazo muhimu. Masomo ya darasani yanaanza saa **moja na dakika thelathini(1:30)** hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwahi shuleni na kushiriki zoezi la usafi ili kuingia darasani kwa muda sahihi.

4.1 MAHUDHURIO

a) Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria shuleni siku zote za masomo.
b) Mwanafunzi anatakiwa kutii kengele mara zote inapogongwa.
c) Ni lazima mwanafunzi ahudhurie vipindi vya dini vya dhehebu lake alilojiandikisha wakati anaingia shuleni, **SI RUHUSA MWANAFUNZI** kubadili **DHEHEBU/DINI** lake/yake hapa shuleni.

d) Ruhusa ya kutofika shuleni siku moja au zaidi itatolewa na **MKUU WA SHULE** au **MAKAMU WA MKUU WA SHULE** na mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anayeruhusiwa kumwombea mwanafunzi ruhusa.**(RUHUSA HAZITOLEWI KWA KUPIGA SIMU SHULENI)**

4.2 JIVUNIE SHULE YAKO.

Mzazi na mwanafunzi wanapaswa kujivunia Shule hii ambayo mwanae anasoma kwa kutaka kujifunza zaidi juu yake. Aidha mzazi/mlezi anakaribishwa kila mara kwa ajili ya kutoa michango ya mawazo yenye nia ya kuboresha uendeshaji wa shule kwa ujumla. ***KWA PAMOJA TUNAIJENGA SHULE YA SEKONDARI KIUSA!***

4.3 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KIKAO MUHIMU CHA WAZAZI:

Kutakuwa na kikao cha wazazi wote wa kidato cha kwanza siku ya Alhamisi ya tarehe 07/01/2021 saa 8:00 Mchana hapa shuleni, tafadhali fika bila kukosa na uwakilishi hauruhusiwi. ZINGATIA MUDA!

KARIBU SANA KIUSA SEKONDARI,

.....
P . J. TEMBA
MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MANISPAA YA MOSHI.

SHULE YA SEKONDARI KIUSA,
S.L.P. 8229,
MOSHI.

TAARIFA ZA MWANAFUNZI.

(Fomu hii ijazwe na mwanafunzi wa kidato cha kwanza na wanafunzi wote wanaohamia)

A. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.

Jina .....
Tarehe ya kuzaliwa .....
Kabila .....
Dini .....
Uraia.....
Jina la Baba .....
Jina la Mama .....
Idadi ya Kaka zake.....
Idadi ya Dada zake.....
Anwani ya nyumbani .....
Namba ya simu .....
Tatizo lolote la kiafya .....

B. ELIMU YA MSINGI.

Shule ya Msingi .....mwaka .....mpaka .....
Shule ya Msingi .....mwaka .....mpaka .....
Shule ya Msingi .....mwaka .....mpaka.....

C. SHULE YA SEKONDARI ULIYOTOKA (Kwa wahamiaji tu).

Jina .....
Anwani .....

Ninathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni sahihi kulingana na weledi wangu.

....
Tarehe Saini ya mwanafunzi.

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

D. Ijazwe na mratibu wa Kidato (Form Coordinator)

Tarehe ya kuandikishwa hapa shuleni .....
Nambari ya usajili .....
Kidato alichoandikishwa .....
Tarehe ya kumaliza shule .....
Kidato cha juu alichofika .....
Namba ya mtihani ya Kidato cha nne .....
Saini ya Mratibu wa Kidato .....
Saini ya Mkuu wa Shule .....
Tarehe .....

Scanned with CamScanner

KIUSA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 8229,
MOSHI.

MEDICAL EXAMINATION FORM.

To be completed by a medical officer

Student's full Name.....

Age.....Sex.....

Blood count (Red and White).....
Stool Examination.....
Urine analysis.....
Sexually Transmitted Diseases.....
TB Test..... Skin.....
Eye Test.....Ears.....
Chest..... Spleen.....
Abdomen.....

ADDITIONAL INFORMATION eg. Physical or chronic family disease(s) etc.
.....
.....

I certify that the above student is fit./unfit to pursue his/ her studies.

Signature.....
Designation.....

Section.....

Signature..... Date.....

Scanned with CamScanner

SHULE YA SEKONDARI KIUSA,

S.L.P. 8229,

MOSHI.

TAREHE.....

HATI YA UTII WA SHERIA.

Mimi Bwana / Bibi ..... Mzazi /Mlezi wa .....

Nimesoma kwa makini sheria za Shule kama zilivyoandikwa na ninazikubali sheria hizo.

Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa mwanangu anaelimishwa na Umma kwa manufaa ya Umma.

.....

SAINI YA MZAZI.

TAREHE.....

Mimi ..... Mtoto wa .....

Nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa na ninazikubali Sheria hizo.

Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa naelimishwa na Umma kwa Manufaa ya Umma.

.....

SAINI YA MWANAFUNZI.

TAREHE .....

Scanned with CamScanner

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI KIUSA,
S.L.P. 8229,
MOSHI.

HATI YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

A. UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi Bwana/Bibi .....Mzazi/mlezi wa mwanafunzi .....wa kidato cha..... mwaka ..... Nilizingatia kuwa Shule zote nchini zinazendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Iwapo mwanangu atashiriki kwenye migomo yoyote, kuchochea na kuongoza vurugu itakayovunja amani na usalama wa shule au kikundi cha watu, achukuliwe hatua za kisheria kulingana na maamuzi ya vikao halali vya kujadili nidhamu vya Bodi ya shule na nitakuwa tayari kutekeleza maamuzi hayo.

Jina la Mzazi .....

Saini ya Mzazi/Mlezi .....

Tarehe .....

B. UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI

Mimi .....Mtoto wa Bwana/Bibi..... ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha..... mwaka ..... katika Shule tajwa hapo juu.

Nitazifuata kanuni na sheria zote za shule na kwamba nimesoma kwa makini Sheria ya Elimu na Shule kama zilivyoandikwa za kutoshiriki migomo yoyote na uchochezi na kuongoza vurugu zitakazovunja amani na usalama katika eneo la shule au kikundi cha watu. Iwapo nitapatikana na makosa hayo, nitakuwa tayari kukubaliana na maamuzi ya vikao vya nidhamu vya Bodi ya shule. Kwa mkataba huu sina budi kutii na kuheshimu maamuzi hayo.

Jina la mwanafunzi .....

Saini ya mwanafunzi .....

Tarehe .....

C. UTHIBITISHO WA UONGOZI WA KATA.

Mimi.....Afisa Mtendaji wa Kata ya.....,..., ninathibitisha kuwa ninamfahamu Bwana/Bibi.....ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi.....wa kidato cha.....mwaka.....aliyetoa uthibitisho huu.

Saini.....Tarehe.....Muhuri.....

Namba ya simu.....

Scanned with CamScanner